# OFISI YA RAIS -TAMISEMI
# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA
# SHULE YA SEKONDARI BUHONGWA

SIMU: 0754581617

Email:

S.L.P 10713,

**MWANZA.**

KUMB. NA. BUH/SS/F.I/J/VOL.I/2023/001 TAREHE: ..................

MWANAFUNZI ............................................................

S.L.P ..........., **MWANZA.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUHONGWA-BWENI WILAYA YA NYAMAGANA MWAKA 2023**

## 01:00: UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2023. Shule ya Sekondari Buhongwa ipo kata ya Buhongwa, Wilaya ya Nyamagana Mkoa wa Mwanza. Usafiri wa basi kutoka mjini kati unapatikana katika Kituo cha Daladala cha Igombe Mkabala na Benki ya Posta na Kituo cha Daladala cha Sahara kwa nauli ya Tsh.500/= hadi Kituo cha Daladala cha Buhongwa. Shule ipo upande wa kaskazini kutoka Kituo cha Daladala Buhongwa takribani umbali wa mita 200.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **09/01/2023.** Hivyo unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe **08/01/2023.** Ufikapo shuleni ripoti Ofisi ya Mkuu wa Shule.

## 2:0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 2:1 SARE YA SHULE

(a) Sare ya shule hii ni suruali ya bluu (Bluu Masai) kwa wavulana. Chini iwe na upana wa sentimeta 19 (miguu isiwe model) na iwe na marinda mawili kila upande. Suruali iwe ndefu ya kugusa viatu. Kwa upande wa wasichana ni sketi ya bluu (Bluu Masai). Iwe na marinda kumi na sita (16), michirizi ya rangi nyeupe 02) mbele kwenda chini na ivuke ugoko. Viatu vyeusi vya kamba kwa wote wavulana na wasichana na soksi nyeupe ndefu kwa wote, Kwa upande wa shati, ni shati nyeupe mikono mifupi kwa wote wasichana na wavulana.

(b) Rangi ya Hijab ifanane na Sare za shule (mshono umeambatanishwa) kwa Waislam tu.

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suite bluu kwa wavulana na track suite blue kwa wasichana.

### 2:2: MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI WA BWENI

- Shuka mbili (02) za rangi ya bluu bahari
- Uje na godoro futi 2 na nusu
- Chandarua nyeupe
- Blanket moja (01), mto na foronya za bluu bahari .
- Gauni la kushindia Bwenini rangi ya **CREAM** kwa wanafunzi wenye ulemavu na rangi ya **PINK** wanafunzi wasio na ulemavu, solo-kitamba cha satini , malapa na toilet papers za kutosha
- Taulo na khanga kwa ajili ya kuogea
- Mafuta ya kupaka ya mgando (Baby Care") kopo 01 kubwa na siyo lotion
- Dawa za meno Pkt 02 kubwa na miswaki 03, sabuni za kuogea 05 na kufulia miche 05
- Nguo za michezo ( track suite rangi ya blue)
- Nguo za kulalia ( night dress)
- Nguo za ndani za kutosha ( shimizi, underskirt n.k)
- Mfagio wa ndani (soft broom) 01
- Mfagio wa nje (chelewa ndefu) 01
- Mfagio wa kusugulia sinki la choo 01
- Vibanio vya nguo



CamScanner

- Ndoo ndogo ya maji ya kunywa na ndoo kubwa ya kuogea na kufulia.
- Vyombo vya chakula sahani,bakuli kijiko na kikombe. Vyombo vya plastic haviruhusiwi.
- Sanduku la Chuma 01
- Njoo na dawa ya viatu, brush, vitana, sweta rangi ya blue, mswaki taa ya betri au solar kwa matumizi yako binafsi ikitokea umeme umekatika. Fedha ya kutosha ya matumizi binafsi na kununulia maji kwa matumizi yake binafsi, pesa hii ikabidhiwe kwa Uongozi wa keupusha wizi.
- Ream double A pc 01

**NB: MWANAFUNZI WA BWENI LAZIMA AJE NA BIMA YA AFYA PAMOJA NA PESA YA KUTOSHA YA MATUMIZI BINAFSI (POCKET MONEY)**

## 2:3: MAELEKEZO MENGINE YA ZIADA YA SHULE

2:3: 1: Shule inafundisha masomo kumi na moja Civics, History, Geography, Kiswahili, English, Physics, Biology, Chemistry, Commerce, Book-keeping na Mathematics njoo na daftari 11 counter books quire 3 na daftari za msomi 11 kwa ajili ya kufanyia mazoezi, kalamu 12 za wino bluu au nyeusi na mathematical Set,Dictionary na any class library reader.

2:3:2 Shule inatoa chakula na Uji kwa wanafunzi wa Bweni tu, wanafunzi wa kutwa watajitegemea wenyewe, kwahiyo mzazi mwenye mwanafunzi wa kutwa hakikisha unampatia mwanao fedha ya chakula na nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani

2:3:3 Ni Jukumu la kila mzazi mwenye mtoto hapa kumtibisha mwanae anapougua akiwa shuleni, hivyo unatakiwa kuweka namba ya simu ya uhakika pindi itokeapo tatizo umuijie.

2:3:4: Tangu mwaka 2018 shule imekuwa ikipokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu (Albino na vipofu) kwahiyo unatakiwa kuwapa ushirikiano wa kiutu hasa wanapohitaji msaada wako wa kimaelekezo.

## 3:0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi wazazi,wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla Ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(g) Kuvaa Sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na Kutunza mali ya umma.

## 3:1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi, Uasherati na ushoga, Ubakaji.
b) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubel n.k
c) Kupigana au kupiga
d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
e) Kudharau bendera ya Taifa
f) Kuoa au kuolewa, Mwanafunzi wa kike kupata ujauzito na Kutoa mimba.
g) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
h) Kukataa adhabu kwa makusudi
i) Mwanafunzi kuwa na simu ya mikononi, kamera, vitu hatarishi mfano kisu,pisipisi n.k
j) Mwanafunzi wa kiume kusababisha mimba kwa mwanafunzi mwenzake wa kike



CS CamScanner

**4:0 MAMBO MENGINE MUHIMU KWA MWANAFUNZI WA BWENI**

A: Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospital ya Serikali Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.

B: Fomu ya maelezo binafisi kuhusu historia ya mwanafunzi,mkataba wa kutoshiriki katika Migomo, fujo na makosa ya jinai.

C: Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni,kulipa ada,michango na maelekezo Mengine yatakayotolewa na shule.

**5:0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU**

Motto wa shule hii ni “Elimu ni Ukombozi” (Education for liberation) Lugha ya Mawasiliano hapa shuleni ni kiingereza tu hivyo anza kufanya mazoezi ya kukiongea.

Jamii ya Shule ya sekondari Buhongwa inawakaribisheni sana.

......................................

SARAH P. LUGUGA SHIMO

**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
BUHONGWA SECONDARY SCHOOL
Box 10713 MWANZA

# HATI YA KUKUBALI KUINGIA KIDATO CHA KWANZA 2023

Mimi ……………………...............………(jina) Nimepokea barua yako ya masharti ya kujiunga na Shule ya Sekondari Buhongwa

Ninaahidi kutii amri zote halali zitakazotolewa na Walimu na walezi wangu wengine shuleni. Nitafanya kazi zote zitakazotolewa na shule yangu na Taifa kwa ujumla.

Nitafanya jitihada katika masomo yangu wakati wowote.

Naelewa kwamba nitakapo kuwa Mwanafunzi sitaruhusiwa kufanya yafuatyo:-

01. Kuvuta sigara au bangi au kutumia madawa ya kulevya
02. Kuoa au kuolewa
03. Kufanya mgomo au kutoshiriki mgomo
04. Kujiunga na makundi ya wahuni au Kufanya makosa ya jinai
05. Kuwa na simu au kisu,pisipisi shuleni n.k
06. Kufanya udanganyifu wa Mtihani (kuibia)
07. Kuvaa mlegezo kwa wavulana/kuvaa sketi fupi inayovuka magoti kwa wasichana
08. Kugombanisha wanafunzi wenzangu/wafanyakazi wa shule kwa uongo au uchochezi
09. Kukwepa vipindi vya masomo yoyote na kutoroka shuleni kabla ya muda muafaka
10. Kuwa nje ya shule bila ruhusa.

Pia naahidi kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za bweni zikiwemo usafi, kuamka mapema, kuwahi muda wamaandalizi darasani usiku na kuwa na ufaulu mzuri kitaaluma kila mwaka.

Sahihi ya uthibitisho wa mzazi/mlezi ………………………………………………………………………

Nakubali na masharti ya shule kama yalivyo orodheshwa hapo juu nikishindwa nifukuzwe shule.

Jina la Mwanafunzi: ………………………………………sahihi ya mwanafunzi……………………….

Jina la Afisa Elimu Kata ………………………. sahihi ….……………... Simu Na. ………………….

Mhuri wa Ofisi yake ……………………………………………………………………………………

CamScanner

# HISTORIA YA MWANAFUNZI

01. Jina la Mwanafunzi ……………………………………………………………………………

02. Shule ya Msingi aliyosomea ………………………………………………………………

03. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………………………...

04. Dini/Dhehebu lake ………………………………………………………………………

05. Jina la Baba (amefariki/yu hai) ……………………………………………………………

06. Jina la Mama (amefariki/yu hai) ……………………………………………………………

07. Anwani ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………..

08. Jina la Mtaa …………Jina la M/kiti wa mtaa……………….............simu ya M/kiti wa Mtaa ……

09. Namba ya Nyumba ……………………………………………………………………………..

10. Jina la Balozi wako ……………………….............Simu ya Balozi wako………………………

11. Kazi ya Mama/mlezi ……………………………….. kazi ya baba/mlezi ………………………..

12. Namba zingine za Familia yako 01. ………………………. Uhusiano ……………………………

02. ………………………. Uhusiano ……………………………

13. Wewe ni mtoto wangapi katika familia yenu …………………………………………………..

14. Wewe ni mtoto wa ngapi kubahatika kupata Elimu ya Sekondari katika Familia ……………..…

15. Jina la Mtu atakaepelekewa ripoti zako za shule ………………………………………………

Anwani yake: ……………………………    Simu yake: ………………………………..

Bandika Picha ya Mwanafunzi Hapa    Bandika Picha ya Mzazi Hapa



CamScanner

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES**
**MWANZA CITY COUNCIL**
**BUHONGWA SECONDARY SCHOOL**

**PHONE: 0754581617**

**Email:**

P.O. BOX 10713,

**MWANZA.**

DAY SCHOLARS' MEDICAL EXAMINATION FORM

THE MEDICAL OFFICER,

……………………………………..

……………………………………..

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name of Pupil ……………………………………………………………………class………………………...
Please examine the above mentioned as to his/her fitness for accommodation in school dormitory

| NO | ITEM | CONDITION | REMARKS |
|---|---|---|---|
| 01. | Mental condition | | |
| 02. | Sight | | |
| 03. | Hearing | | |
| 04. | Chest TB | | |
| 05. | Urine | | |
| 06. | Stool | | |
| 07. | Widal test | | |
| 08. | Blood BP,HB | | |

Any other physical disability not listed that may affect his/her studies at school

………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………..

Signature ……………………………………………………………… Date ………………………………...

Medical Officer ………………………………………………………...

Official Stamp …………………………………………………………



CamScanner

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES**
**MWANZA CITY COUNCIL**
**BUHONGWA SECONDARY SCHOOL**

## AFFIDAVIT

I am ………………………………………………………. Tanzania do here make that and states as follows:-

I ……………………………………. I am the ………………………... (Father, Mother of Relative)
Of ……………………………………………. that the said ……………………………………………..
Was born at ………………………………………………………………………………………………..

(Incase of affidavit being sworn by her relative – not being parent)
…………………………………………………………………………… on account of …………….
Describe the circumstances id such personal and direct knowledge of the said ………………………
Was a Girl/Boy

Signed …………………………………………………………………………………………………….

Sworn at …………………………………………………………………………………………………..

This ………………………………………………………….          Day of …………………………..

To …………………………………………………………….

Name ………………………………………………………..

Qualification ………………………………………………..

Address ……………………………………………………..

Signature ……………………………………………………

(Official Stamps if Seal)
(& Delete whichever is inapplicable)



CamScanner